



GRETSA UNIVERSITY-THIKA

**UNIVERSITY EXAMINATIONS
JANUARY - APRIL 2021 SEMESTER**

**DIPLOMA IN JOURNALISM AND MASS
COMMUNICATION**

COURSE CODE: DJMC 037

**COURSE TITLE: KISWAHILI FOR JOURNALISTS AND
WRITERS**

DATE: 11 MAY 2021

TIME: 8:00 AM – 11:00 AM

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

1. SECTION A IS **COMPULSORY**.
2. SECTION B: ANSWER ANY OTHER **THREE** QUESTIONS.
3. **DO NOT** WRITE ANYTHING ON THIS QUESTION PAPER AS IT WILL BE AN EXAM IRREGULARITY.
4. ALL ROUGH WORK SHOULD BE AT THE BACK OF YOUR ANSWER BOOKLET AND CROSSED OUT.

CAUTION: *All exam rooms are under CCTV surveillance during the examination period.*

SEHEMU YA A: SWALI LA LAZIMA

- a) Uakifishaji ni kipengele muhimu katika uandishi na uhariri wa habari. Dhihirisha hili kwa kuweka alama za uakifishi zifaazo kwenye habari iliyoko hapa chini, kisha uiandike kwa usahihi kwenye kijitabu chako cha majibu. **[Alama 10]**
- b) katibu mkuu wa tawi la machakos la chama cha walimu wa shule za upili na vyuo hapa nchini kuppet musembi katuku ametoa wito kwa serikali kuwa makini inapotafakari kufungua upya taasisi za masomo akihutubia wanahabari mjini machakos katuku alisema ni mapema zaidi kutafakari kuhusu uwezekano wa kufunguliwa kwa shule wakati huu ambapo visa vya ugonjwa wa korona vimeongezeka hapa nchini katuku alisema serikali badala yake inafaa kuimarisha juhudi za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo
- c) Eleza umuhimu wa alama za uakifishi huku ukitoa mifano mbalimbali. **[Alama 10]**
Fafanua dhana zifuatazo:
- i. Mtindo **[Alama 5]**
 - ii. Regista/sajili **[Alama 5]**
 - iii. Simo (jargon) **[Alama 5]**
 - iv. Lahaja **[Alama 5]**

SEHEMU B: JIBU MASWALI YOYOTE MATATU

SWALI LA PILI

- a) Baadhi ya waandishi wa habari/watangazaji wamelaumiwa kwa kukiuka kanuni za lugha ya Kiswahili. Jadili. **[Alama 10]**
- b) Kiswahili kinanufaika sana kutokana na jukumu linalotekelezwa na vyombo vya habari katika kukikuza, kukiendeleza na kukisambaza. Fafanua. **[Alama 10]**

SWALI LA TATU

- a) Jadili umuhimu wa uteuzi wa maneno (diction) katika unadishi wa habari. **[Alama 5]**
- b) Eleza hatua tatu zifuatazo za maandalizi ya uandishi:
- i. Utafutaji wa mada **[Alama 5]**
 - ii. Upangaji wa mawazo **[Alama 5]**
 - iii. Utafiti **[Alama 5]**

SWALI LA NNE

Jadili umuhimu wa istilahi zifuatazo katika uandishi.

- i.** Uradidi **[Alama 5]**
- ii.** Hadhira **[Alama 5]**
- iii.** Lengo **[Alama 5]**
- iv.** Akronimu **[Alama 5]**

SWALI LA TANO

- a)** Eleza hatua tatu muhimu za mchakato wa uandishi wa habari. **[Alama 10]**
- b)** Sarufi ina dhima kuu katika uandishi. Jadili. **[Alama 10]**

SWALI LA SITA

- a)** Muongozo wa kazi na nidhamu (Code of ethics) huzuia waandishi wa habari kukiuka mipaka ya kazi. Jadili. **[Alama 10]**
- b)** “Msomaji wa habari ndiye mhariri wa mwisho katika mchakato wa kukusanya na kuwasilisha habari.” Fafanua. **[Alama 10]**